

Pambazuko

Toleo Namba 172

Jumatatu, Julai 6-12, 2026

TPA yapata boti za kisasa kuimarisha ulinzi Uk. 13


TEC haina nia ovu na Samia

● Ni kauli ya Askofu Niwemugizi anayesema mengi katika mahojiano maalum



Uk. 6&7

Baraza la maaskofu tuna wajibu wa kinabii, tunapaswa kuzungumza, kuelimisha pamoja na kuombea nchi yetu, lakini tuna wajibu pia wa kufundisha mambo yaweje kwa kuzingatia ukweli,”



Tahariri

Tusiruhusu yeyote kuchezea amani ya Tanzania

KAMWE Tanzania siyo shamba la majaribio ya chuki na haiwezi kuwa uwanja wa kuchezea amani iliyopo.

Nchi yetu siyo taifa la kuachwa mikononi mwa watu wanaotaka kupanda mbegu za uhasama, vurugu na mgawanyiko kwa maslahi yao binafsi.

Tahariri Uk. 2

Chokochozo zakemewa, ulinzi waimarishwa Dar

Uk. 14



Hatari: 'Energy drinks' zimejaa viambata vya dawa za kulevya

Habari Uk. 12

Zungu: Nchi haijengwi kwa maandamano

SPIKA wa Bunge Mussa Azzan Zungu amesema nchi haiwezi kujengwa kwa kutupiana maneno wala maandamano.

Habari Uk. 15



■ Tahariri

Tusiruhusu yeyote kuchezea amani ya Tanzania

KAMWE Tanzania siyo shamba la majaribio ya chuki na haiwezi kuwa uwanja wa kuchezea amani iliyopo.

Nchi yetu siyo taifa la kuachwa mikononi mwa watu wanaotaka kupanda mbegu za uhasama, vurugu na mgawanyiko kwa maslahi yao binafsi.

Amani ya nchi hii ni tunu kubwa, iliyojengwa kwa jasho, busara, uvumilivu na hekima ya vizazi vilivyotangulia. Kwa hiyo, yeyote anayethubutu kuivuruga amani ya Tanzania, kwa kauli, vitendo, propaganda au uchochezi, lazima akemewa kwa nguvu zote.

Sisi Pambazuko tunasema wazi kwamba mtu anayechochea Watanzania wagombane, haitakii mema nchi hii. Anayegeuza siasa kuwa sumu ya kuwatenganisha wananchi, haitakii mema Tanzania. Anayetumia dini, kabila, ukanda au tofauti za kiitikadi kuwachonganisha watu, huyo ni adui wa ustawi wa taifa, hata kama anavaa koti la uzalendo au demokrasia.

Tunaamini kuwa vyama vya siasa siyo kiwanda cha chuki. Siasa ni ushindani wa hoja, sera na maono; siyo uwanja wa matusi, vitisho, uongo na uchochezi. Hakuna chama chenye thamani kuliko Tanzania. Hakuna kiongozi mkubwa kuliko taifa. Na hakuna tamaa ya madaraka inayostahili kulipwa kwa kuvuruga amani ya wananchi.

Wanaotaka kutimizwa kwa madai yao, ni vyema wakajenga hoja, siyo kujenga makundi ya chuki. Watafute ridhaa ya wananchi, siyo kuwatisha au kuwagonganisha.

Tanzania imebarikiwa kuwa na watu wengi wanaofuata vyema imani zao za dini, makabila na tamaduni nyingi, lakini tumbaki kuwa taifa moja kwa sababu tulikataa sumu ya ubaguzi.

Ndiyo maana tunasema kwa msisitizo; dini zisitumike kuleta vurugu. Nyumba za ibada

zisiwe majukwaa ya kugawa taifa. Mimbari zisitumike kupandikiza chuki.

Kiongozi yeyote wa dini anayechochea uhasama anapaswa kukemewa bila woga, kwa sababu dini ya kweli hujenga utu, upendo na maridhiano; haichochei maangamizi.

Pia, wanasiasa nao wasijenge daraja la chuki kwa kuwa na kauli za kuchochea na kuharibu utangamano wa wananchi wetu ambao wamekuwa wakiishi kwa utulivu wa kutosha kwa miaka mingi.

Aidha, mitandao ya kijamii isiwe dampo la uchafu wa fikra. Wanaosambaza maneno ya chuki, video za uchochezi, taarifa za uongo na ujumbe wa kugawa Watanzania wanapaswa kujua kuwa wanachezea moto wenye hila ya kugawa taifa.

Tanzania inapovurugika kwa kuchochewa vurugu, madhara hayatachagua chama, dini, cheo wala kabila. Vurugu zikianza, hazimuulizi mtu alimchagua nani. Zinabeba kila mtu.

Kwa hiyo, wajibu wa kuilinda Tanzania siyo wa serikali pekee, ni wa kila raia mwenye akili timamu na mapenzi ya kweli kwa nchi yake. Tukiona dalili za uchochezi, tukemee. Tukisikia kauli za kugawa watu, tuzikatae. Tukikutana na wanasiasa, wahubiri au wanaharakati wanaochezea amani, tuwaambie wazi; Tanzania siyo mali yao.

Katika nchi hii, amani kwanza; utulivu kwanza; utaifa kwanza na kwamba bila amani, hakuna demokrasia. Bila utulivu, hakuna maendeleo. Bila mshikamano, hakuna kesho.

Tanzania yetu lazima ilindwe kwa wivu mkubwa, kwa sababu tukiruhusu wachache wenye tamaa wamvuruge mama huyu, historia haitatusamehe na madhara yake ni makubwa yatakayohukumu kila mwenye hila ya kuvuruga.

Zawadi kwa Rais Msumbiji... ■



Rais Samia Suluhu Hassan akimkabidhi zawadi mgeni wake, Rais wa Msumbiji, Daniel Francisco Chapo wakati wa ufunguzi wa Maonyesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam juzi. (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

■ Dunia: Hapa na Pale

Muhoozi aburutwa kortini

WAKILI mwandamizi wa Kenya, Martha Karua, amemfungulia kesi Mkuu wa Majeshi wa Uganda, Jenerali Muhoozi Kainerugaba, akipinga hatua ya kuzuiwa kuingia nchini humo na kurejeshwa Kenya.

Karua, ambaye pia ni kiongozi wa chama cha People's Liberation Party (PLP), alikuwa sehemu ya jopo la mawakili wa mwanasiasa mkongwe wa upinzani Uganda, Dkt. Kizza Besigye, na mwenzake Obeid Lutale.

Katika hati yake, Karua anasema alikuwa na kibali maalumu cha uwakili kilichotolewa na Uganda Law Council, hivyo kuzuiwa kwake kuliathiri haki ya wateja wake kupata utetezi wa kisheria.

Hatua hiyo imeibua mjadala mpana kuhusu utawala wa sheria, uhuru wa mawakili na nafasi ya jeshi katika masuala ya kiraia nchini Uganda.



Albania bado yachemka

WANANCHI wa Albania wameendelea kuandamana jijini Tirana kwa siku ya 35 mfululizo, wakipinga rushwa, matumizi mabaya ya Madaraka.

Maandamano hayo, yaliyoanzia katika upinzani dhidi ya mradi wa hoteli ya kifahari kwenye eneo la hifadhi ya pwani linalohusishwa na familia ya Rais wa Marekani, Donald Trump, sasa yamegeuka kuwa vuguvugu pana dhidi ya serikali ya Waziri Mkuu Edi Rama.

Waandamanaji wamekuwa wakitaka Rama ajiuzulu, kufanyika kwa mageuzi ya kikatiba na uchunguzi huru wa tuhuma za rushwa.

Katika maandamano hayomaelfu ya watu walio kuwa wakielekea eneo maarufu la Skanderbeg Square wamekuwa wakipaza sauti kwa kuimba; "tunataka Albania mpya" na kukemea kile wanachokiiita ufisadi wa watawala. Polisi wameendelea kuwatawanya, lakini wamekuwa wakirejea kila mara.



Khamenei azikwa bila mtoto

KIONGOZI wa sasa wa Iran, Mojtaba Khamenei, jana hakuhudhuria maziko ya baba yake, Ayatollah Ali Khamenei, yaliyofanyika jijini Tehran, hali iliyoi-bua maswali kuhusu usalama wake na mwenendo wa uongozi mpya nchini humo.

Taarifa zinaeleza kuwa Mojtaba, ambaye ameripotiwa kujificha tangu mashambulizi yaliyomuua baba yake, hakuruhusiwa kujitokeza hadharani kutokana na hofu ya kushambuliwa tena.

Hata hivyo, ndugu zake wawili walihudhuria ibada na shughuli za maziko, pamoja na viongozi waandamizi wa serikali na jeshi.

Kutokuwepo kwake kumeongeza minong'ono kuhusu hali yake kiafya, usalama wake binafsi na uthabiti wa uongozi wa Iran katika kipindi cha mvutano mkubwa wa kisiasa na kijeshi.

China yamwachia mchungaji

CHINA imemwachia huru Mchungaji Ezra Jin Mingri, kiongozi wa Kanisa la Zion, baada ya kushikiliwa kwa miezi kadhaa katika kile wanaharakati wa haki za kidini walichokitaja kuwa sehemu ya msako dhidi ya makanisa yasiyosajiliwa rasmi.

Jin, ambaye alikamatwa Oktoba mwaka jana pamoja na viongozi wengine wa kanisa hilo, ameripotiwa kuwasili jana Los Angeles, Marekani, na kuungana tena na familia yake.

Kuachiwa kwake kumekuja wiki chache baada ya Rais Donald Trump kulizungumzia suala lake katika mazungumzo na Rais Xi Jinping.

Hata hivyo, wanaharakati wanasema baadhi ya waumini wa Kanisa la Zion bado wanashikiliwa nchini China.



Karne ya kupiga kofi ichochee kuwajibika kwa wabunge wetu

BUNGE la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linapojiandaa kutimiza miaka 100 Januari mwakani, 2027, kuna kila sababu ya kupiga kofi.

Karne moja siyo mchezo. Ni umri wa babu mwenye hadithi nyingi, makovu mengi, kumbukumbu nyingi na bila shaka, ahadi nyingi ambazo nyingine bado anakumbuka ama asikumbuke kutokana na umri.

Nilikuwa miongoni mwa wazee walioalikwa kusikiliza simulizi ya safari hii ndefu ya Bunge. Spika Mussa Zungu alizungumza kwa kujiamini kwamba Bunge la wananchi ambalo sasa analisimamia yeye, linafanya vizuri zaidi kuiwajibisha serikali.

Akasema katika kipindi chake, yapo mengi ambayo wabunge wameyakataa, serikali ikasikiliza, ikayaondoa au kuyarekebisha kwa ajili ya kuleta unafuu na neema kwa Watanzania.

Kwa hilo, ninampa hongera zake Spika Zungu na kwa wawakilishi wote, lakini kwa sababu kwa hulka, umri wangu na makuzi yangu, sija-lelewa na kufunzwa kupiga vigelegele, naomba nimhoji Spika Zungu kuhusu utendaji wa bunge la sasa. Je, anatambua wananchi wengi wanalizungumzia vipi bunge analoongoza?

Endapo hana taarifa, anitafute tukae kitako nimpe taarifa za uhakika kuhusu mtazamo wa wananchi kuhusu yeye na pia wabunge anaawaongoza.

Ni kweli, Bunge likikataa jambo baya na serikali ikalisikiliza, hiyo ni afya ya demokrasia. Ni kweli, mbunge akisimama na kuhoji kwa nia-ba ya mkulima, mfanyakazi, mfanyabiashara, mama lishe, mwalimu na mgonjwa anayekosa dawa, hapo Bunge linakuwa Bunge kweli.

Lakini Bunge likigeuka kuwa ukumbi wa kusifiana, kutazamana usoni na kupima uzito wa hoja kwa rangi ya chama, hapo karne moja inaweza kuwa mapambo ya kalenda tu.

Bunge la miaka 100 halipaswi kujivunia tu idadi ya vikao, hotuba, kanuni na sherehe. Lina-

paswa kujipima kwa kiwango cha machozi yaliyofutwa. Linapaswa kujiuliza; Ni bajeti ngapi zimekataliwa na baadaye kurekebisha kwa neema ya nchi na watu wake?

Lijiulize, je, ni mikataba mingapi imepelekwa mezani kwa wabunge na wao “kuichanachana” kabla ya kusainiwa? Ni mawaziri wangapi wamewajibishwa siyo kwa kelele, bali kwa ushahidi? Ni ahadi ngapi za serikali zimefuatiliwa hadi mwisho?

Ninaposema Bunge liwajibishe serikali, simaanishi bunge liwe adui wa serikali. Hapana, ninataka kuona linakuwa daktari wake. Daktari mzuri hakupigi kofi kwa sababu una homa kali; anakupima, anakuchoma sindano na kukuambia ukweli hata kama unauma. Serikali nayo ikikosea, Bunge lisiipe peremende, kiipe dawa.

Ndiyo maana maneno ya Spika Zungu yanahitaji kubebwa kama ahadi, siyo kuwa hitimisho. Kama kweli serikali inasikiliza Bunge, basi wananchi wanahitaji kuona hilo kwenye bei ya maisha, huduma za afya, ajira za vijana, maji, barabara, elimu na haki.

Ni vyema uwajibikaji wa bunge na mawaziri usiishie kwenye kumbukumbu rasmi za majadiliano bungeni – hansard, unatakiwa kushuka hadi sokoni, kijijini na hospitalini.

Miaka 100 ya Bunge iwe sherehe ya kujitazama kwenye kioo, endapo Bunge letu liko vyema lijipongeze nasi tupongeze, kama kuna vumbi, tufute na ikiwa kuna doa, tusiweke poda; tulisafishe.

Wakati Bunge letu likifika miaka 100, lisijisifu tu kwa kuzeeka, lijisifu kwa kuwa na meno ya kuuma hoja mbovu, macho ya kuona mate-so ya wananchi na moyo wa kusimama upande wa wananchi, bila kuonea serikali.

Haya yakifanyika, hata mimi na uzee wangu nitasimama na kujipiga kifua na hata kofi kwamba chombo chetu kinafanya kazi ya kutukuka

■ Habari Kuu

TEC haina nia ovu na Rais Samia



Askofu wa Jimbo Katoliki, Rulenge-Ngara

Na Mwandishi WETU, Ngara

ASKOFU Jimbo la Rulenge-Ngara, Kagera, Dkt. Severine Niwemugizi amesema Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) halina nia ovu kwa Rais Samia Suluhu Hassan, hasa pale linapokosoa serikali anayoongoza.

Kwamba TEC inapokosoa jambo inafanya hivyo kwa kutimiza wajibu wake wa kinabii unaowataka kuzungumza, kuelimisha na kufundisha kwa kuzingatia ukweli.

Aidha, TEC kamwe haina lengo baya na mtu yeyote isipokuwa kuhimiza haki, wajibu na utumishi kwa umma.

Katika mahojiano maalum na Pambazuko kwenye makazi yake ya Uaskofu yaliyopo Ngara Mjini, Kagera hivi karibuni, Dkt. Niwemugizi pamoja na mambo mengine, amesema viongozi wa TEC wanafuata mwongozo katika kujadili

mambo ya kijamii na hawaendi nje ya hapo katika kufanya utume wao.

Amesema TEC ina zaidi ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwake hapa nchini, ikiwa ni taasisi ya dini ambayo ni sauti ya wasio na sauti na muda wote imekuwa ikizungumza pale inapoo-na mambo hayaendi sawa.

“TEC haina ubaya wowote na Rais Samia, isipokuwa tu sisi hukutana na kujadili hali ya kijamii, hali ya kisiasa, hali ya kiuchumi inavyokwenda na kanisa kama taasisi lina wajibu wa kuzungumza, kama raia yeyote mwenye haki ya kuzungumza juu ya nchi yao...”

“Baraza la maaskofu tuna wajibu wa kinabii, tunapaswa kuzungumza, kuelimisha pamoja na kuombea nchi yetu, lakini tuna wajibu pia wa kufundisha mambo yaweye kwa kuzingatia ukweli,” amesisitiza.

Baadhi ya wanasiasa, wakiwamo viongozi wa chama tawala, wamesikika wakieleza kuwa yapo matamko ya TEC yenye viashiria vya kulaumu na kushutumu uongozi wa Rais Samia.

Pia, Desemba 2, mwaka jana – 2025, Rais Samia akizungumza na wazee wa Dar es Salaam alikemea baadhi ya viongozi wa dini na taasisi zao kwa matamko ambayo alisema; “Hatujaipa dini yoyote mamlaka ya kutoa tamko la ku-override (kubatilisha) mengine,” alisisitiza na kuongeza; “Tanzania hatutaendesha na madhehebu ya dini.”

Rais Samia akasema; “Matamko manane yametolewa na TEC, lakini ukienda chini wenyewe wanapingana. Waliosimama kwenye haki wanaona ni batili iliyofanyika,” alisema Rais Samia.

Maswali na majibu

Swali: Tanzania ina miaka minne kuelekea uchaguzi mkuu, lakini joto la kisiasa ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) limeanza kupanda. Unaitathmini vipi hali ya mshikamano wa kitaifa, amani na utulivu wa kisiasa nchini katika mazingira kama haya?

Habari Kuu ■

TEC haina nia ovu...

Inatoka Uk. 6

Jibu: Mimi siyo mwanasiasa, na siyo mtaalam wa sayansi ya siasa, lakini niko ndani ya jamii, naweza kusikia watu wanazungumza nini, wanasemasema nini, hali ikoje kwa ujumla, CCM mimi siko ndani, lakini ninaona mshikamano wa kitaifa wenye mashaka.

Watu sasa hawaaminiani, hata ndani ya CCM wao hawaaminiani, mengine ni kauli, zinazotolewa hata ndani ya bunge, watu wanaitana wasaliti.

Unaona kama hapa kuna shida, ukisikia wanazungumza masuala ya Muungano, kubagua na unaona ipo shida.

Wanasiasa hawakosi cha kuzungumza, wanaweza kuzungumza kwa ujumla, lakini kwa undani huoni kama kuna utulivu kweli wa kisiasa. Ile amani ya kweli mimi nina mashaka na siwezi kusema ninaionja amani ya kweli katika mazingira ya sasa.

Kuna mwingine amesema watu sasa hivi wamenyamaza, wako kimya, lakini ndani wananung'unika, kungekuwa na chombo cha kuwatazama ndani mioyoni na akilini mwao, ungeona kwamba watu wengi hawaridhiki, ingawa wanaweza kuonyesha nyuso za tabasamu, kucheka, lakini kwa ndani sidhani kama kuna utulivu wa kweli, amani kamili.

Swali: Kumekuwa na mijadala na mitazamo tofauti kuhusu kupungua kwa nafasi ya mijadala ya kisiasa na uhuru wa vyama vya siasa. Je, kama kiongozi wa dini unaona mazingira ya sasa yanatoa fursa sawa kwa wadau wote kushiriki katika kujenga Taifa?

Jibu: Ninafikiri kuna kukwepa mijadala, kwa sababu ya hali halisi ya kiusalama, watu wanaogopa kuzungumzia mambo yalivyo halisi, kwa sababu ukizungumzia mambo kwa uhalisia, unajua kinachofuata ni nini.

Kwa hiyo fursa ya kweli ya watu kushiriki katika kujenga taifa letu sasa hivi ninaona kwamba fursa hizi si sawa. Kwa maana ya kwamba, kuna wenye haki ya kuongea na wasio na haki ya kuongea.

Ukiongea katika mazingira ya sasa bila kupongeza, kusifu, basi wewe unaambiwa siyo mzalendo, ukijaribu kuona hapa kuna mapungufu fulani, ingekuwa hivi... ingekuwa vizuri zaidi..unaambiwa wewe si mzalendo.

Sasa katika hali ya namna hiyo mtu unakosa ujasiri wa kutoa maoni ya kujenga, kama hauogopi kuhatarisha maisha yako.

Kwa hiyo hii inaondoa kabisa hiyo fursa ya watu katika kuchangia mawazo ya kujenga taifa lao, badala ya kuona kwamba yule anayetoa maoni tofauti na ya kwako anataka kukupa njia ya kutengeneza vizuri zaidi au uende njia nzuri zaidi kuliko ile unayoifuata.

Ukiitoa hiyo wewe unaonekana ni adui wa taifa, sasa kwa mtindo huo hatuwezi kushiriki sawa katika kujenga taifa letu.

Swali: Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimekuwa kikilalamikia kuzuiwa kufanya shughuli zake za siasa kwenye baadhi ya maeneo, unadhani ni nini kifanyike ili kuhakikisha ushindani wa kisiasa unafanyika kwa haki?

Jibu: Mimi nisingezungumzia Chadema peke yake, nizungumzie hali nzima ya mitazamo tofauti kwamba vyama vyote vingepaswa kuwa na haki sawa, viruhusiwe kuzungumza.

Ninachokiona ni kwamba kwanza, sheria zirekebishwe kwa sababu mambo yote yanaongozwa na sheria.

Sasa zile sheria za hila zirekebishwe, zile zinazowafanya wengine waonekane ukisema hivi wewe ni mhaini, ukisema hivi...wewe huna nia njema, huna heshima nakadhalika, hizo ziondolewe.

Watu walioendelea wanaruhusu watu kuzungumza, kutoa maoni, mimi nimekuwa nasikiliza Marekani, Uingereza, ukisikiliza lugha nyingine unaziogopa kwelikweli, ni lugha kali. Lakini huko watu wameshajenga ukomavu, ukomavu uliowapa usugu wa kuchuja na kusikiliza kwamba hii lugha kwa wengine ni tusi, lakini kwa mwingine hili tusi silijali, lakini kuna hisia fulani, kuna jambo lolote la maana huko linalotoka ambalo unaweza kusema hapa kuna jambo lolote la maana naweza kulichukua.

■ Habari Kuu



Askofu wa Jimbo Katoliki, Rulenge-Ngara akiwa katika picha ya pamoja na Mhariri Msanifu wa Gazeti la Pambazuko, Arodia Peter baada ya mahojiano maalum yaliyofanyika jimboni kwake mkoani Kagera hivi karibuni. (Picha na Mpigapicha Maalum).

TEC haina nia ovu...

Inatoka Uk. 7

Hata kama aliyelitoa kalitoa kwa lugha isiyo ya staha sana. Saa nyingine wanasema lugha ya staha, sawa unajua tumeumbwa tofauti. Kuumbwa tofauti kuwe ni kama zawadi hivi, hata kichaa anaweza kuzungumza kitu kina maana.

Sasa chuja uone lipi la maana ambalo linanaisaidia mimi katika kuleta kwa mfano mema ya wengi, uchafu achana nao.

Sisi hatujafikia ukomavu huo, ndiyo maana kuna sheria za kufunga watu wasizungumze, wasitoe maoni. Mimi nafikiri tuondoe sheria za hila.

Sheria za hila mimi ndiyo nazilaumu kabisas, zinawafanya wengine wawekwe kando, kwa sababu pamoja na hizo sheria zenyewe kuna wengine pamoja na kwamba wanaweza kuwa

wanafanya makosa yaleyale, mfano vyama vya upinzani au vyenye maoni tofauti wanafanya yale ambayo yanaonekana kufanywa na wengine yaonekane ni tusi.

Kwa hiyo vyama vinatendewa tofauti.

Sasa tukiwa na vipimo tofauti vinavyotofautiana katika jambo lilelile naona hapo hatupeani fursa zilizo sawa.

Swali: Unazungumziaje utendaji wa vyombo vya habari katika ujenzi wa maendeleo ya taifa kwa sasa?

Jibu: Vyombo vya habari vimekwisha kabisas, naweza kusema kwamba ndani ya miaka sita hadi saba hivi, vyombo vya habari vyote vinatikiwa viwe vya kusifu, kupongeza serikali na siyo kufunua yale yasiyo sahihi watu wakayajua.

Ukishayafunua hayo, chombo cha habari kesho kinafungiwa, kwa hiyo vyombo vya habari sasa hivi vimefungiwa kabatini, vinatumika tu kwa wale wenye mamlaka, kile kinachotoa kitu ambacho hakimpendezi mwenye mamlaka basi siyo cha kizalendo, kinaonekana kipo kuchochea na lugha zinazofanana na hiyo.

Lakini kwakweli mahala ambapo watu wanataka maendeleo, vyombo vya habari vinakuwa na uhuru. Mimi naamini wanaoendesha vyombo vya habari wana ujuzi, wanajua miiko, maadili na miiko, vikiachiwa vizungumze yale yanayokuwa ya ukweli, tungepiga hatua kubwa.

Swali: Kumekuwepo na malalamiko ya mara kwa mara kuhusu vitendo vya utekaji, kupotea kwa watu, na ukiukwaji wa haki za binadamu nchini. Ukiwa kiongozi wa kiroho, una ujumbe gani kwa serikali, vyombo vya dola na wanchi kuhusu suala hili?

Jibu: Hili ni kati ya sababu za mtanziko na mtikisiko katika taifa letu, hili jambo halileti afya katika taifa letu, haya matukio tumeanza kuyasikia miaka michache iliyopita lakini sasa yamekuwa ndiyo mtindo wa maisha.

Watu kukaa na hofu, chombo cha dola kinaonekana kama vile ndiyo hatari kabisa, sasa hatuwezi kwenda namna hiyo, ninavyofahamu, serikali na vyombo vya dola kazi yake ni kulin-da maisha ya watu na mali zao.

Inaendelea Uk. 9

TEC haina nia ovu...

Inatoka Uk. 8

Watu wajisikie huru wakiona polisi yuko pale, wangejisikia wako salama, lakini kwa sasa hivi mtu unakuwa na mashaka, ukimuona polisi hapo unashtuka, hivi niko kwenye kosa au niko salama?

Kwamba muda wowote naweza kupotea, sasa kwa mwendo huo hauleti afya kwenye jamii zetu. Hivyo nafikiri serikali lazima irudi kwenye nafasi yake na kujiuliza kwa nini jamii ina picha hii?.


Inapicha gani na sisi?, kwa nini kila mara yanayoripotiwa watu wanasema waliokuja kufanya jambo hili ni jeshi la polisi?. Na kama si kweli, polisi imefanya nini kurekebisha hali hili?.

Kwa mfano, mtu aliyekamatwa na kufungwa pingu, akawekwa kwenye gari, halafu bodaboda wakafuatilia hilo gari, katika mazingira ambayo tunaambiwa huyo mtu kafaule kuchomoka kwenye hilo gari halafu akaonekana baada ya kupita kwenye msitu.

Sasa kama wewe ndiyo mwenye ufunguo, ni nani anaweza kuwa na pingu akaweza kumfunga mtu, kama siyo polisi? labda kama kuna duplicate ambapo mtu mwingine asiye polisi anaweza kuzitumia kumteka mtu na baadaye anasema njoo tukufungue, sasa utamwaminije huyo mtu?

Wiki ijayo tutakuwa na simulizi namna Askofu Dkt. Niwemugizi alivyoulizwa na Rais John Magufuli, "wewe ni raia"? Na siku mbili baadaye alipokonywa hati yake ya kusafiria.

Dkt. Nchimbi ateta na Warioba...



Makamu wa Rais Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi akiwa na Waziri Mkuu Mstaafu Jaji Joseph Warioba alipomtembelea kumjulia hali katika makazi yake, Mbezi Juu jijini Dar es Salaam juzi. (Picha na Ofisi ya Makamu wa Rais).

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

Jamani msimuonee bure Katambi

NI Wajaluo tu ambao huwa wanasimamisha saa ili kuokoa muda wasichelewe wanakoenda. Katambi siyo mmoja wao. Yeye ni Msukuma getegete.

Naweza kueleza kwamba tatizo siyo Katambi. Tuna mgongano sugu kati ya majasusi wanasiasa na wanasiasa majasusi. Hawa ni watu wawili tofauti.

Nitaeleza siku nyingine kuhusu hili. Na niseme tu kwamba endapo mnaoogopa kuchanganya dini na siasa, ogopeni pia kuchanga ujasusi na siasa.

Kuna mambo tisa yanayozua maswali:

Kwamba Paschal Chinyele (jasusi mwanasiasa), kamrushia mpira Spika (Mwongozo). Spika akatuliza kifuani. Akampasia mpira Katambi (mwanasiasa jasusi). Katambi akajifunga goli kwa kuinuka na tamko la serikali. Imekaa saa ngapi? Kama ilikaa kwa nini wampange Paschal na Spika? Wameuza mechi.

Kwamba zuio la mikutano likatolewa bunge. Tuseme ni bunge limezuia mikutano?

Kwamba limetamkwa na waziri; Tuseme ni waziri kazuia? Aliishapiga chanjo ya kumkinga na kirusi cha kuvunja katiba?

Kwamba waziri katamka neno eti kwa niaba ya Amiri Jeshi, Je, ni rais kazuia kupitia waziri, tena kupitia mhimili mwingine? Msimchonganishe rais wetu na wananchi.

Kwamba IGP kaagizwa kukiuka katiba. Atatii? Akitii, nani mkosaji? Aliyeagiza au aliyetii?

Kwamba kwa nini waziri hakusubiri waziri mkuu ndiye atoe zuio hilo kwa niaba ya serikali wakati anaahirisha bunge?

Kwamba kwa nini serikali isitumie TCD au Msajili wa Vyama Tanzania, wakitwa wadau na kushawishiwa wakubaliane kuvunja katiba?

Je, ili zuio au katazo la mikutano au zuio ama katazo la kutumia katiba; yaani kwamba imeenda likizo kwa muda?! Hatua hii hufanyika nchi ikiwa vitani au wale jamaa zangu majirani wa Wajaluo wanapoamua kuchanganya cha Arusha na siasa. Sasa tunaomba katiba mpya ya nini ikiwa iliyopo haina kazi mpaka inaenda likizo?!

Sasa iko hivi; je, mikutano ya kisiasa ni haki ya kikatiba au ni fadhila za serikali kwa wananchi? Tafadhali, nimeuliza kwa upole tu.

Hapa nashauri; Kwa kuwa umeanza kama mchezo wa kuigiza, tujifanye igizo limeisha, tundelee na mishe mishe zetu za weekend.

Halafu; msiende kubugudhi wageni kwenye hoteli usiku wakati wa doria. Mtaona yasiyowahusu. Ishia mapokezi kwa kunyata. Kama kuna Mjalu anataka kuandamana, subiri kupambazuke, mdake Tanganyika jeki hata kama Tanganyika haipo, mpeleke kwa Polisi siyo Safe House.

Kikubwa naomba makatazo haya yaishie hapo kwenye siasa. Msiguse mikutano ya dini, harusi, jando wala Yanga atakapomfunga Simba.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Patrobas Katambi

Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba

Taswira ya Dar kwa sasa ni usalama au hofu?

KATIKA siku za hivi karibuni jijini Dar es Salaam, taswira na mazingira yaliyopo yamenifanya nita-fakari zaidi.

Ukipita katika jiji letu hili, karibu kila njia panda kuna askari wenye silaha wanaoonekana kuwa tayari kwa mapambano.

Pia yapo magari ya polisi yenye taa zinazowaka katika maeneo mengi yakinguruma bila kuzimwa kwa muda wote.

Hali hii ilianza kidogo kidogo katika maeneo machache, lakini kwa siku za hivi karibuni tunaona ni sehemu nyingi zaidi.

Ni kweli kuwa vyombo vya usalama vina jukumu la msingi kulinda raia na mali zao, lakini tafakari inakuja kwa kujiuliza taswira hii inatuma ujumbe gani kwa wananchi na hata kwa wageni walioko jijini hapa?

Pamoja na taswira hiyo, tumesikia vilevile Waziri wa Mambo ya Ndani, Patrobas Katambi aki-toa katazo la uwepo wa mikutano ya kisiasa, swali linakuja tena kulikoni?

Usalama ni nguzo muhimu ya maendeleo. Ustawi wa taifa hutokana na utulivu na amani. Kwa hali hiyo uwepo wa polisi na vyombo vingine vya usalama ni jambo la kawaida kwa nchi yoyote.

Hata hivyo, ni vyema tujue kuwa usalama haupimwi tu kwa idadi ya askari wanaoonekana mitaani wakiwa na silaha za kivita.

Kipimo cha usalama hakiwezi kuwa kiwango ambacho watu wanajisikia salama, huru na wenye imani na taasisi zinazowalinda.

Taswira ya jiji hili ina athari kubwa kwenye saikolojia ya jamii. Mtoto, mfanyabiashara, mwekezaji au mtalii anapooona askari wenye silaha na muonekano wa utayari wa mashambulizi na magari ya doria kila kona, anaweza kujiuliza iwapo kuna tishio la kiusalama ambalo haliko wazi.

Kwa upande mwingine, wapo wanaoweza kuona hiyo ni ishara ya umakini wa dola katika kulinda usalama, lakini hapohapo wapo wanaoweza kupata hisia za hofu au wasiwasi.

Mitazamo yote hiyo ipo na ndiyo maana ni

muhimu kutafakari namna hatua za kiusalama zinavyoonekana machoni mwa umma kabla ya kuwaweka askari wanaoonekana wakiwa tayari kwa mapambano.

Kwa wakati tulionao kwa sasa duniani humu, usalama haujengwi kwa nguvu pekee. Usalama unaweza kujengwa kwa uaminifu kati ya vyombo vya dola na wananchi.

Wananchi wakiwa na imani kwamba taasisi za dola zinawalinda kwa haki, uwazi na weledi, hisia za usalama huongezeka hata bila uwepo wa askari wengi wenye silaha mitaani.

Vinginevyo, mazingira yanayoweza kutafsiriwa kuwa ya tahadhari ya kudumu yanaweza kuibua maswali ambayo hayakuwepo.

Mfano tunapomsikia waziri akitoa tamko ambalo kwa wanasheria tunahoji uhalali wake, inazidisha hali ya sintofahamu kwenye uhalisia wa usalama wa nchi.

Tunaweza kusema kuwa Jiji la Dar es Salaam ndiyo lango la nchi. Ndipo wageni wengi huliona kwanza wanapowasili nchini.

Taswira yake ni sura ya taifa. Inafaa kila hatua ya kuimarisha usalama izingatie pia ujumbe unaopeleka kwa kwa wananchi, wawekezaji na watalii.

Wananchi wasibaki na maswali ya kutaka kujua kwani kuna nini mbona jiji kama limezingirwa vile? Usalama unaonekana unapaswa kwenda sambamba na usalama unaohisiwa.

Lengo la tafakari hii siyo kupuuza umuhimu wa vyombo vya usalama, ila inabidi tufahamu kuwa jamii yenye amani siyo ile inayowaona askari kila mahali, bali ni ile ambayo wananchi wake wanaiishi bila hofu, wakiadini kuwa sheria na taasisi za umma zipo kwa ajali ya kuwalinda wote kwa usawa.

Usalama hautapimwa kwa wingi wa silaha mitaani, misingi ya kiusalama inatakiwa isizue hofu wala wasiwasi.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwana-harakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.

■ Habari

Hatari: 'Energy drinks' zimejaa viambata vya dawa za kulevya

Na Mwandishi WETU

IMEBAINIKA kuwa baadhi ya vinywaji vya kuongeza nguvu vilivyokuwa na kemikali ya THC, ambayo ni kiambata kinachopatikana kwenye bangi, kina madhara mbalimbali ikiwemo kuathiri afya ya akili.

Hilo limebainishwa wiki iyopita na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Meneja Ukaguzi na Utekelezaji wa Sheria kutoka TBS, Nuru Ediga Mwasulama amesema wataendelea kushirikiana na DCEA kuhakikisha bidhaa zilizothibitishwa ikiwemo virutubisho vya vyakula hazitakuwa kibebeo cha dawa za kulevya.

Meneja huyo amesema tayari wamewapatia mafunzo maofisa wao nchi nzima, ili kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya.

Kwa upande wake Meneja wa Ukaguzi na Udhibiti wa TMDA, Emmanuel Mkiligi amesema wataendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kubaini makundi yanayojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya.

"Pia tutahakikisha tunashirikiana na DCEA na mamlaka mbalimbali kuwa bidhaa za dawa zitatumia kwa taratibu zinazotakiwa," amesema Mkiligi.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo akizungumzia kuhusu operesheni mbalimbali zilizofanyika nchini kati ya Mei na Juni mwaka huu, wamewakamata watumishi wa serikali



sita waliokuwa wakisaidia kusafirisha dawa za kulevya.

"Wanne kati ya hao sita, tumewafikisha mahakamani na wawili tunaendelea kuchukua hatua ili waweze kufikishwa mahakamani..."

"Kinachofanyika ni kwamba kwa kuwa ni watumishi wa serikali, wanaweza kusaidia wale wahalifu kuwafikisha mahali fulani, wakijua kwamba kule barabarani wanaposimamishwa na kutambulisha na kuonyesha vitambulisho wanaweza kupita bila kukaguliwa..."

"Kutokana na hilo, sasa tutahakikisha kwamba watumishi wote na wasafirishaji wa dawa za kulevya na magari yote yanayopita hata akitambulisha yeye ni nani itabidi sasa tuanze kukagua hayo magari au huyo anayesafiri," amesema Kamishna Lyimo.

Amesema wamebaini pia watumishi wa serikali wanaotumia dawa hizo za kulevya, ambapo wanatumia maeneo ya starehe ya VIP na nyumba za kupanga.

"Kwa Jiji la Arusha zinatumiwa kumbi za starehe kwenye maeneo ya VIP, kwa Dar es Salaam wanakodi hizi apartment na kumbi za starehe kwenye hayo maeneo ya VIP kufanya matukio hayo," amesema.

Aidha, amesema kwa kuwa tayari wame-shabaini hayo maeneo wataendelea kufanya ugakuzi.

Kamishna Lyimo, amesema DCEA imeweka mikakati ya kukabiliana na usafirishaji wa dawa za kulevya kupitia virutubisho vya chakula, dawa na kemikali kwa kufanya ukaguzi na operesheni katika maeneo mbalimbali.



TPA yapata boti za kisasa kuimarisha ulinzi

Na Mwandishi WETU

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imenunua boti mbili za kisasa za doria ziendazo kwa kasi, zenye thamani ya dola za Marekani milioni 6.445, ikiwa ni hatua ya kuimarisha usalama wa shughuli za kibandari, kulinda shehena za wateja na kuongeza ufanisi katika usafirishaji wa majini.

Boti hizo, MV LINDO I na MV LINDO II, ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa TPA unaolenga kuhakikisha bandari za Tanzania zinakuwa salama, za kisasa na zenye uwezo wa kukidhi viwango vya kimataifa katika ulinzi wa meli, mizigo, watumiaji wa huduma za bandari na miundombinu ya kimkakati.

Imeelezwa kuwa MV LINDO I itatumika kufanya doria katika Bandari ya Dar es Salaam na maeneo ya fukwe zinazozunguka ukanda huo, wakati MV LINDO II ikipelekwa kuimarisha ulinzi katika Bandari za Ziwa Victoria pamoja na maeneo ya fukwe zinazohudumia bandari hizo.

Boti hizo zimejengwa kwa teknolojia ya kisasa na zina uwezo wa kukimbia kwa kasi ya knots 35, hali inayozifanya kufika haraka kwenye maeneo yenye dharura, kufanya doria za mara kwa mara na kukabiliana na matukio yanayoweza kuhatarisha usalama wa bandari, meli na shehena.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mkurugenzi wa Huduma za Meli

na Shughuli za Kibandari, Nahodha Abdulla Mwingamno, alisema uwekezaji huo unaonesha dhamira ya mamlaka hiyo ya kujenga bandari salama, shindani na zenye kuaminika.

“Kupatikana kwa boti hizi kutaimarisha usalama wa watumiaji wa bandari, meli na shehena za wateja zikiwa melini na bandarini. Aidha, zitaongeza uwezo wetu wa kufanya doria, kukabiliana na matukio ya dharura na kudhibiti vitendo vya wizi, udokozi na magendo,” alisema Nahodha Mwingamno.

Maana kubwa ya hatua hii ni kwamba TPA haitazami usalama kama suala la ulinzi pekee, bali kama sehemu muhimu ya biashara. Bandari inapokuwa salama, wafanyabiashara hujenga imani zaidi, meli huongezeka, shehena hupita kwa uhakika na huduma hutolewa kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Aidha, uwekezaji huu utasaidia kupunguza hatari za uhalifu wa majini, kulinda mizigo ya wateja, kuimarisha udhibiti wa maeneo ya fukwe na kuongeza uwezo wa askari wa TPA kufanya ufuatiliaji katika maeneo mapana zaidi.

TPA imesema ununuzi wa boti hizo unaenda sambamba na maboresho mengine ya usalama, ikiwamo matumizi ya zaidi ya kamera 480 za ulinzi katika Bandari ya Dar es Salaam na maeneo mengine. Hatua hizi zinaifanya Tanzania kuwa na bandari salama, zenye ushindani na mchango mkubwa zaidi katika ukuaji wa uchumi wa taifa.

■ Habari

Chokocho zakemewa, ulinzi waimarishwa Dar



Na Mwandishi WETU

ULINZI umeimarishwa zaidi katika Jiji la Dar es Salaam kufuatia taarifa za kuwepo maandamano yaliyofurushwa na serikali.

Tahadhari hiyo ya kuhakikisha amani inatamaliza inaonekana kuwepo kwa idadi kubwa ya askari wa Jeshi la Polisi, pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

Pambazuko limeshuhudia uwepo wa idadi kubwa ya magari yakiranda katika mitaa na Barabara za Dar es Salaam na tangu jana ulinzi mkali umeimarishwa katika Viwanja vya Sabasaba.

Katika viwanja hivyo, shughuli za biashara zinaendelea katika Maonyesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara maarufu Sabasaba.

Ulinzi huo umeonekana kwa wananchi wanaoingia katika viwanja hivyo ambao kabla ya kuingia viwanjani hapo wanakaguliwa na askari Polisi ambao wanatumia vifaa maalumu.

Ukaguzi huo ulionekana kufanywa na askari wa vyeo vya chini na wale wenye nyota mbili ambao walikuwa wakisimamia ukaguzi huo kwa umakini mkubwa.

Wadadisi wa mambo wanabashiri kwamba ukaguzi huo unafanyika kama njia ya kutoruhusu uvunjifu wowote wa amani kufanyika.

Katika hatua nyingine tahadhari ya kuwepo kwa maandamano kumeleta hofu na wasiwasi kwa wananchi ambao wamejihami kwa kuchukua tahadhari kubwa.

Baadhi ya wananchi hao hivi sasa wamehamisha familia zao hasa watoto na kuwapeleka nje ya Dar es Salaam kwa kile wanachodai kujihami na rabsha zinazoweza kutokea.

Kutokana na uwepo wa taarifa za maandamano hayo, tayari askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na lile la Polisi na mengine wameweka ulinzi wa kutosha kila kona ili kuyadhibiti.

Kadhalika, magari ya majeshi hayo yameonekana yakitanda katika njia kuu na Barabara za kawaida Jiji la Dar es Salaam ili kulinda ulinzi na usalama.

Wanaharakati kwa kutumia mitandao ya kijamii, wamekuwa wakihamasisha kuwepo kwa maandamano ambayo wanadai yanasukuma ajenda yao ya kudai katiba mpya.

Wanaharakati hao, wengi wakiwa nje ya Tanzania wamekuwa wakitangaza kuwa kesho – Jumatane; Julai 7, ndiyo siku ya kufanyika maandamano hayo.

Tayari JWTZ imetoa tamko ikiwatahadharisha wananchi kutojitokeza kuandamana vinginevyo wakikaidi watachukuliwa hatua za kisheria.

“Hali ya mipaka ya nchi na usalama nchini ni shwari hali hiyo imechangiwa na wananchi kulinda na kudumisha amani na moyo wao wa kizalendo katika kushirikiana na vyombo vya ulinzi wa usalama...”

“Utulivu na amani umewezesha wananchi kuendelea na shughuli zao za ujenzi wa taifa, ingawa kumekuwa na baadhi ya watu kufanya uhamasishaji na upotoshaji unaofanywa na wasioitakia mema nchi kwa kutaka kushiriki katika vurugu na uvunjifu wa mani na utulivu,” amesema Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano wa JWTZ, Sylvester Mangule.

Amebainisha kwamba watu ambao wanafanya upotoshaji huo kwa kulihusisha jeshi kwamba litawalinda wafanya vurugu, amehimiza kuzikataa na kwamba wananchi wasijitokeze kunga mkono maandamano hayo yenye viashiria vya vurugu.

Zungu: Nchi haijengwi kwa maandamano

Na Hellen NGOROMERA

SPIKA wa Bunge Mussa Azzan Zungu amesema nchi haiwezi kujengwa kwa kutupiana maneno wala maandamano.

Zungu amesema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari kuhusu maadhimisho ya miaka 100 ya chimbuko la Bunge la Tanzania.

“Hatuwezi kujenga nchi kwa maandamano, hatuwezi kubadilisha Katiba ya nchi bila Bunge, fursa ya kuingia ipo kwa kila mmoja na hakuna bunge dhaifu, ukiona watu wanapigana humo ndani ujue hilo siyo bunge, hiyo ni klabu ya Chibuku,” amesema Zungu.

Spika amesema wanaodai kuwa bunge la sasa analoongoza ni dhaifu na halina msisimko, wanashindwa kuelewa kuwa ndani ya chombo hicho cha kutunga sheria, wabunge wanachua-na kwa hoja na kwamba mwenye hoja ya maana anaungwa mkono na hatimaye kufanyika kwa uamuzi wa pamoja bila kujali vyama wanavyotoka.

Amemtaja Mbunge wa Tunduru Kaskazini (ACT Wazalendo) Ado Shaibu kwamba ameku-wa akileta hoja ambazo nyhingine zimeungwa mkono kwa maslahi ya Watanzania wote.

“Bungeni mnakaa mnapingana kwa hoja, Ado ameleta hoja zaidi ya 18 na zilijibiwa na Waziri wa Fedha, namsifu sana Ado kwa hoja zake,” amesema Zungu.

Serikali inasikiliza

Kuhusu matumizi ya magari ya kifahari kwa viongozi wa serikali, Spika Zungu amesema Bunge lilitoa maelekezo kwa serikali kuondokana na matumizi ya magari an serikali imeridhia.

“Hatugombani na serikali, tunatoa maelekezo na sababu, sisi ndio watetezi wa wanachi tunakwenda kwa hoja, hoja inaletwa na kujibiwa. Serikali ipunguze gharama kwa magari ya kifahari mimi nikiwa jimboni natembea na hard top, yote ni katika kupunguza matumizi

“Rais ameshaonyesha mfano kwa kupunguza gharama kwa magari kwenye msafara wake na watendaji wake sasa wanatembea kwa mabasi, sisi wengine tunasubiri nini,” amehoji Spika.

Pamoja na mambo mengine amesema wametoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba Tanzania (NHC) kujenga nyumba zenye gharama nafuu kwa manufaa ya wananchi.

“Tumetoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa NHC pamoja na kujenga nyumba za gharama kubwa ambazo ndizo zinazowapa faida, waanze kujenga za gharama ndogo kwa wananchi wetu...”

“Hawa wataenda kutekeleza hay ana nime-waambia kwamba kuna nyumba zinajengwa kwa milioni 13 hadi 15 na hayo ndiyo maelekezo ya Rais Samia,” amesema Zungu.

Miaka 100 ya Bunge

Kuhusu maadhimisho ya miaka 100 ya chimbuko la Bunge la Tanzania ambayo kilele chake kitakuwa Januari, 2027, Zungu amesema katika kipindi hicho cha uhai wa bunge, mambo mengi makubwa yamefanyika na kutekelezwa na serikali.

Amesema takwimu zinaonyesha kuwa uwakilishi wa wanawake katika Bunge umeongezeka na kwa sasa wanawake wako takribani asilimia 40, kiwango ambacho ni juu ya wastani wa dunia wa uwakilishi wa wanawake wa asilimia 27.5.

Amewahakikishia Watanzania kuwa Bunge limejizatiti kuendelea kusimamia ustawi wa wananchi kwa kuimarisha utendaji kazi wa Bunge.

“Tukio hili linalokuja la miaka 100 ya Bunge, hali- ishii kusherehekea urithi wake pekee, bali pia linathibitisha kujitolea kwetu katika kujenga mustakabali imara, jumuishi zaidi na wa kidemokrasia.



■ Habari

Wizara yasisitiza elimu ya fedha

Na Mwandishi WETU

BAJETI ya mwaka huu wa fedha – 2026/27, imepangwa kumwezesha mwananchi kiuchumi, ikilenga kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Mwaka 2050 kupitia kuimarisha sekta binafsi, kukuza elimu ya juu, na kuongeza uelewa wa masuala ya fedha na kodi kwa umma.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Fedha, Mhandisi Mshamu Ali Munde, wakati akizungumza na vyombo vya habari, alipotembelea banda la Wizara ya Fedha, katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yanayofanyika katika viwanja vya Mwalimu J.K. Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Munde alisema maonyesho ya mwaka huu yameonyesha mafanikio makubwa katika matumizi ya mifumo ya kidijitali na maboresho ya huduma, mambo ambayo ni nguzo muhimu kusogeza huduma za kifedha karibu zaidi na jamii

na kurahisisha shughuli za kiuchumi nchini.

“Wizara ya Fedha imeweka mkazo mkubwa katika kuongeza pato la Taifa na pato la mtu mmoja mmoja kama msingi muhimu wa maendeleo endelevu, ikiwa ni pamoja na kufikia uchumi wenye thamani ya dola trilioni moja na pato la mtu mmoja mmoja kufikia dola 7,000 ifikapo mwaka 2050,” alisema Munde.

Aidha, aliwahimiza wananchi kuachana na mifumo ya fedha isiyo rasmi na badala yake watumie taasisi rasmi za kifedha katika shughuli zao za kila siku, hatua inayolenga kuongeza usalama wa fedha zao, uwazi, na kuleta ufanisi wa jumla katika mifumo ya kifedha nchini.

Alisema wizara pamoja na taasisi zake, inaendelea kutoa elimu ya huduma za fedha pamoja na elimu ya kodi kwa wananchi waliotembelea maonesho hayo waweze kuepuka mikopo isiyo rasmi ijulikanayo kama mikopo umiza ili kuendana kikamilifu na mikakati ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya 2050.

“Kuna umuhimu wa kuendelea kuboresha mifumo ya utoaji wa huduma za fedha ili kuongeza uwajibikaji na ufanisi, jambo linalotazamiwa kuwa chachu ya ongezeko la pato la mwananchi mmoja mmoja na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi,” alisisitiza.

Pia, Munde alipongeza wizara pamoja na taasisi zake kwa hatua kubwa zilizofikiwa katika utoaji wa elimu kwa wananchi katika maonesho hayo na kuisitiza kuendelea kufanya maboresho ili kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakuwa bora zinazokidhi mahitaji ya wananchi kwa ufanisi na kuchangia moja kwa moja katika kukuza pato la taifa.

Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) yanayofanyika katika Viwanja vya Mwalimu J.K. Nyerere, jijini Dar es Salaam, kuanzia Juni 28 hadi Julai 13, yenye Kaulimbiu ya “Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba ni Fahari ya Tanzania”, yanaambatana na kuadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwake.



Mhandisi
Mshamu Ali
Munde

Tanzania kuwa kitovu cha masoko ya hisa

Na Joseph MAHUMI

SERIKALI imejipanga kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha huduma za kifedha, masoko ya mitaji na uwekezaji katika Afrika.

Mipango ya kufanikisha jambo hilo inajikita kuitumia Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) ambalo lina nafasi muhimu ya kuwa mfano kutokana na mafanikio makubwa inayoendelea kupata.

Hayo yamesema na Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar, wakati wa maadhimisho ya miaka 30 ya Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yenye kaulimbiu; “Miaka 30 ya Kuchochea Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uwekezaji Endelevu”, iliyoifanyika jijini Dar es Salaam.

Balozi Omar alisema tangu kuanzishwa kwa DSE, soko hilo limekua kutoka kuwa taasisi yenye shughuli chache za uwekezaji na kuwa moja ya nguzo muhimu za mfumo wa kifedha nchini kwa kuwezesha kampuni, serikali na taasisi zake kupata mitaji ya muda mrefu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

“DSE imechangia kuimarisha uwazi, utawala bora wa kampuni, nidhamu ya kifedha na kuongeza ushiriki wa wananchi katika umiliki wa uchumi kupitia uwekezaji kwenye hisa, hati fungani za serikali na kampuni, pamoja na mifuko ya uwekezaji” alisema Balozi Omar.

Aidha, alieleza kufurahishwa na ongezeko la matumizi ya teknolojia katika uwekezaji, hususan kupitia huduma ya Hisa Kiganjani, ambayo imeongeza ushiriki wa wananchi katika soko la mitaji na kuimarisha ujumuishaji wa kifedha.

Balozi Omar aliongeza kuwa, serikali imeendelea kunufaika na maendeleo ya soko la mitaji kupitia uhamasishaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, akitolea mfano Hati Fungani ya Miundombinu ya Samia, Hati Fungani ya Stawi ya TCB Bank pamoja na Hati Fungani ya Kijani ya Tanga Uwasa. Aidha, Waziri Omar alisema utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2025-2030 unahitaji sekta imara ya fedha na masoko ya mitaji yenye uwezo wa kukusanya akiba za muda mrefu na kuzielekeza katika uwekezaji wenye tija kwenye sekta za kimkakati.



Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar (kulia), akipokea tuzo maalumu ya kutambua mchango wake katika Sekta ya Fedha, kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Peter Nalitolela, katika hafla ya Maadhimisho ya Miaka 30 ya soko hilo. Wengine katika picha ni Mwenyekiti wa Bodi ya DSE, Daniel Ole Sumayan (kushoto nyuma) na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), CPA Nicodemus Mkama (katikati). (Picha na Mpigapicha Wetu).

“Nawataka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) pamoja na wadau wa sekta hii kuendelea kuimarisha mazingira ya maendeleo ya soko la mitaji kwa kuboresha mifumo ya udhibiti, kulinda maslahi ya wawekezaji, kurahisisha taratibu na kuhakikisha soko linaendelea kuwa la uwazi, ufanisi na kuamini-ka” alisema Balozi Omar.

Alihimiza Benki Kuu ya Tanzania (BoT), CMSA, DSE na taasisi nyingine husika kuendelea kuimarisha elimu ya fedha na uwekezaji kwa wananchi ili kujenga jamii yenye utamaduni wa kuweka akiba, kuwekeza na kushirikikikamilifu katika umiliki wa uchumi wanchi. Kwa upande wao, Mwenyekiti wa Bodi ya DSE, Daniel Ole Sumayan na Ofisa Mtendaji Mkuu wa DSE, Peter Nalitolela, walisema katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, DSE imebadilika kutoka taasisi iliyokuwa ikitegemea ruzuku ya serikali kwa asilimia 100 hadi kuwa kampuni inayojitegemea kifedha.

DSE sasa inapata faida na kuipa serikali gawio kila mwaka tangu ilipoorodheshwa katika soko la hisa mwaka 2016.

■ Barua za Wasomaji



Tunakaribisha barua. Tuma kupitia

Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz

Viongozi watathmini maagizo wanayotoa

Mhariri,

AGIZO lililotolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani, Patrobas Katambi kwamba wamiliki wa nyumba za wageni, wahakikishe wateja wao wanaandikishwa kwa kutumia Vitambulisho vya Taifa (NIDA), siyo sawa kwa sababu watu wengi bado hawana vitambulisho hivyo.

Hii ni kwa sababu hadi sasa ni takribani Watanzania milioni 17 ndiyo wenye vitambulisho hivyo.

Nadhani ni busara viongozi wakathmini kwa kina athari za maagizo wanayoyotoa na siyo kuzungumza kwa mihemko au kwa malengo wanayojua wao.

Baadhi ya viongozi wenye kutangaza makatazo hawatendi haki wananchi, sasa kama kati ya Watanzania zaidi ya milioni 60, wenye vitambulisho hivyo ni milioni 17, hawaoni kama italeta athari na usumbufu mkubwa?

**Happy Shao,
Dodoma.**

Kuna uchakachuaiji ujazo wa mitungi ya gesi

Mhariri,

MITUNGI ya gesi ya ujazo wa kilo 15 zamani ilikuwa ikidumu kwa muda mrefu kulingana na matumizi yake, lakini kwa sasa tunashangazwa kwani huisha haraka.

Mara ya kwanza nilipoenda kulalamika kwa wakala, akasema pengine haikufungwa vizuri lakini ilipoisha haraka tena kwa mara ya pili, wakala alikiri kuwa wateja wengi wanalalamika.

Tunaomba hizi kampuni za biashara ya gesi ya kupikia kama kuna kitu wamefanya waache maana itakuwa haina tofauti na wizi.

**Shabani Yasin,
Kigamboni,
Dar es Salaam.**

Mabasi ya Abood mjirekebishe

Mhariri,

NAOMBA unisaidie kuchapisha kero hii ili wahusika waifanyie kazi.

Juni 29, 2026 nilisafiri na basi la Kampuni ya Abood lenye namba za usajili T273EAV lililotokea Bukoba saa 11 jioni kuelekea Dar es Salaam.

Hata hivyo, tofauti na ninavyoyafahamu mabasi ya kampuni hiyo, nilishangazwa na hali

ya uchafu niliouona, chini ya siti, kwenye korido la katikati kulikuwa na uchafu ulioshikana na vumbi, jambo ambalo linaashiria kuwa basi hilo halikufanywa usafi wa kutosha kabla ya kuanza safari.

Vilevile kava za siti zimechakaa hazipendezi wala hazifai kwenye ulimwengu wa usafiri wa kisasa.

Ni mwito wangu kwamba wahusika watarekebishe hali hiyo, mara wasomapo barua hii.

Ni vyema mabasi yanayosafiri mwendo mrefu, ambayo yanatumia viyoyozi yawe yanafanywa usafi kabla ya kuanza safari ili kuwakinga abiria wake na changamoto za kiafya ikiwemo mafua, vikohozi na hata pumu.

Msafiri wa mara kwa mara

Wazo Binafsi ■

Simulizi ya G55 Chaumma inapokuwa somo la sayansi ya siasa

Na Steven MBOGO

‘MAPINDUZI mengi hayafi kwa sababu yanakosa maadui; hufa kwa sababu yanashindwa kuishi na marafiki zao.’

Katika historia ya siasa, kuna nyakati ambazo matukio yanavuka mipaka ya vyama na kuwa masomo ya falsafa ya uongozi.

Mgogoro unaoendelea kuzunguka kundi lililjulikana kama G55, na safari yake inaendelea kutoka Chadema hadi Chama cha Ukombozi wa Umma (Chaumma).

Hatimaye sintofahamu iliyomkumba mmoja wa watu wake muhimu, katibu mkuu na mgombea urais wa chama hicho, Salum Mwalimu, ni miongoni mwa matukio yanayostahili kutazamwa kwa jicho hilo.

Ni rahisi kuugeuza mjadala huu kuwa wa hisia; nani anamsaliti mwenzake? Je, Salum Mwalimu aliwasaliti wenzake wa G55? Au wao ndio waliomsaliti baada ya kumfikisha kileleni?

Lakini maswali hayo, ingawa yanasisimua kisiasa, yanaweza kutuficha swali kubwa zaidi; je, tatizo lilikuwa watu, au mantiki ya mamlaka ndani ya taasisi za kisiasa?

G55 hawakuzaliwa ndani ya Chaumma, walitoka Chadema baada ya chama hicho kupitisha mkakati wa kisiasa wa “No Reforms, No Election” kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Kwa mtazamo wa kundi hilo, kushiriki uchaguzi, licha ya mapungufu yaliyokuwapo katika mfumo wa uchaguzi, kulionekana kuwa njia bora ya kuendelea kuwasilisha sauti ya upinzani na kuendelea kujenga ushawishi wa kisiasa. Kwao, kususia uchaguzi kulibeba hatari ya kukiacha chama nje ya uwanja wa ushindani wa kisiasa.

Tofauti hiyo ya kimkakati ilikuwa mpaka kuwa tofauti ya kisiasa. Baadhi ya wanachama waliokuwa sehemu ya G55 walijiondoa Chadema na baadaye kujiunga na Chaumma huku

wakibeba matumaini kwamba chama hicho kingekuwa jukwaa jipya la kutekeleza maono yao ya kisiasa.

Kwao safari hiyo haikuwa tu kuhama chama; ilikuwa jaribio la kuthibitisha kwamba tofauti ya kimkakati haipaswi kuwa mwisho wa ndoto ya kisiasa.

Ndani ya Chaumma kumetokea mgogoro wa kiuongozi uliosababisha vyombo vya chama kuchukua hatua dhidi ya Salum Mwalimu.

Kamati Kuu ilipitisha azimio la kutokuwa na imani naye baadaye baraza kuu likaridhia hatua za kumwondoa katika nafasi yake.

Mwanasosholojia na mwanafalsafa wa siasa, Max Weber aliwahi kutofautisha aina mbili za maadili katika uongozi; kiongozi anaweza kushikilia msimamo kwa nguvu kwa sababu anaamini ndiyo kweli, au anaweza kufanya maamuzi kwa kuzingatia athari zake kwa taasisi na jamii.

Mara nyingi, migongano mikubwa ya kisiasa huzaliwa pale ambapo viongozi wawili wanadhani wanailinda taasisi moja, lakini kila mmoja anatumia aina tofauti ya maadili ya kiuongozi.

Huenda baadhi ya waliokuwa G55 waliamini wanaitetea roho ya mageuzi yaliyowakusanya. Huenda pia viongozi wa Chaumma waliamini wanailinda taasisi ya chama dhidi ya kile walichokiona kuwa ukiukaji wa utaratibu. Hivyo, mgongano haukuwa tu wa watu; ulikuwa mgongano wa tafsiri mbili kuhusu maana ya uaminifu kwa taasisi.

Lakini je, migogoro kama hii ni ajali, au ni sehemu ya asili ya siasa zenyewe? Swali hilo linatufikisha kwenye nadharia nyingine maarufu katika sayansi ya siasa, ambayo huenda ndiyo inaeleza vizuri zaidi hatima ya makundi mengi yanayozaliwa kwa ari ya mageuzi.

Mwandishi wa makala haya ni mtafiti, mchambuzi wa mambo ya jamii, siasa na uchumi

■ Historia

Benazir Bhutto mwanamke jasiri aliyekifuata kifo



Na The CONNECT

KWENYE ulimwengu wa siasa unaotawaliwa na wanaume, hasa katika mataifa ya Kiislamu ya Mashariki ya Kati na Asia ya Kusini, jina la Benazir Bhutto linasimama na kuwa muhanga wa demokrasia.

Alikuwa mwanamke wa kwanza katika historia kuchaguliwa kuongoza taifa la Kiislamu akiwa Waziri Mkuu wa Pakistan.

Hata hivyo, jina la familia yake; Bhutto lilikuwa kama laana iliyobeba baraka za madaraka makubwa, lakini likilipwa kwa gharama ya damu.

Benazir Bhutto alizaliwa tarehe 21 Juni 1953 mjini Karachi, Pakistan. Alikuwa binti mkubwa wa Zulfikar Ali Bhutto, mwanasiasa nguli na Waziri Mkuu wa zamani wa Pakistan aliyependwa sana na wananchi.

Benazir alilelewa katika maisha ya kifahari na akapata elimu ya kiwango cha juu duniani katika vyuo vikuu vya Harvard (Marekani) na Oxford (Uingereza), ambako alijifunza falsafa, siasa, na uchumi.

Ndoto zake za kuwa mwanadiplomasia wa kawaida zilizimika ghafla mwaka 1977. Jenerali Muhammad Zia-ul-Haq aliipindua serikali ya baba yake kupitia mapinduzi ya kijeshi. Baba yake, Zulfikar, alikamatwa na baada ya kesi ya utata, alinyongwa mwaka 1979.

Kifo cha baba yake kiligeuka kuwa cheche iliyomuingiza Benazir kwenye ulingo wa siasa. Alilitazama jeneza la baba yake na kuapa kuen-deleza mapambano ya kidemokrasia, huku yeye na mama yake wakichukua uongozi wa chama cha Pakistan Peoples Party (PPP).

Uamuzi wa kusimama dhidi ya dikteta Zia-ul-Haq ulimgharimu sana Benazir. Alitumia miaka mingi chini ya vizuizi nyumbani na kwenye jela zenye joto kali na mazingira magumu ya Pakistan, ambapo afya yake ilidhoofika. Baadaye ilimbidi kukimbilia uhamishoni nchini Uingereza.

Mwaka 1988, baada ya Jenerali Zia-ul-Haq kufariki kwenye ajali ya ndege, milango ya demokrasia ilifunguka. Benazir alirudi Pakistan, ambapo maelfu ya wananchi walimimini-ka barabarani kumpokea kama mkombozi.

Katika uchaguzi wa mwaka huo, akiwa na umri wa miaka 35 tu, Benazir Bhutto alichaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa Pakistan. Alikuwa mwanamke wa kwanza kuongoza nchi ya Kiislamu, tukio lililoshtusha na kuhamasisha ulimwengu mzima. Aliongoza kwa vipindi viwili tofauti (1988–1990 na 1993–1996).

Benazir Bhutto...

Inatoka Uk. 20

Ingawa alikuwa kipenzi cha maskini, vipindi vyake vya utawala viligubikwa na vita kali ya kisiasa na tuhuma za ufisadi zilizomhusisha mume wake, Asif Ali Zardari (aliyeitwa “Mr. 10%”). Hii ilisababisha serikali yake kuangushwa mara zote mbili na jeshi, na kumfanya akimbilie uhamishoni Dubai 1999.

Baada ya miaka minane uhamishoni, Oktoba 2007, Benazir Bhutto aliamua kufanya uamuzi wa hatari zaidi katika maisha yake.

Licha ya kupokea ripoti za kiintelijensia kutoka mashirika ya siri ya magharibi (kama CIA) kuwa vikundi vya kigaidi vya Al-Qaeda na Taliban vilikuwa vimepanga kumuua pindi akirudi, alisimamia msimamo wake wa kurudi kupigania demokrasia dhidi ya utawala wa kijeshi wa Jenerali Pervez Musharraf.

Siku ileile aliyotua mjini Karachi Oktoba 18, 2007, msafara wake ulishambuliwa na mabomu mawili ya kujitoa muhanga katikati ya umati wa watu waliokuwa wanamshangilia. Zaidi ya watu 140 walifariki dunia papo hapo. Benazir alinusurika kifo hicho kimuujiza, lakini badala ya kukimbia nchi, aliangalia damu ya wafuasi wake na kusema: “Sitarudi nyuma. Maisha yangu si kitu mbele ya uhuru wa Pakistan.”

Ilikuwa ni jioni ya Desemba 27 2007, kwenye bustani ya kihistoria ya Liaquat National Bagh mjini Rawalpindi (mji uleule ambao baba yake alinyongwa miaka 28 iliyopita). Benazir Bhutto alikuwa amemaliza kuhutubia mkutano mkubwa wa kampeni za uchaguzi uliogusa mioyo ya maelfu ya wafuasi wake.

Baada ya hotuba, aliingia ndani ya gari lake la kuzuia risasi aina ya Toyota Land Cruiser ili kuondoka. Hata hivyo, kutokana na mapenzi makubwa kwa watu wake waliokuwa wakigonga vioo vya gari na kumlilia, Benazir aliamua kufungua sehemu ya juu ya paa la gari ile (sun-roof) na kusimama ili kuwapungia mkono na kutabasamu kwa mara ya mwisho.

Katika sekunde hiyo ya hatari, kijana mmoja mshambuliaji aliyekuwa mita chache kutoka



kwenye gari alichomoa bastola na kufyatua risasi tatu kuelekea kwake. Risasi zilimfika shingoni na kifuani, na kumfanya aanguke ndani ya gari. Sekunde moja baadaye, mshambuliaji mwingine alijilipua kwa bomu kubwa lililoua watu wengine 20 waliokuwa karibu.

Benazir alikimbizwa hospitali, lakini majeraha yalikuwa makubwa mno. Mnamo saa 12:16 jioni, madaktari walitangaza rasmi kuwa Benazir Bhutto amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 54.

Kifo chake kilisababisha machafuko, simanzi, na kilio nchini Pakistan na kulaaniwa kote ulimwenguni. Alizikwa pembeni ya kaburi la baba yake huko Garhi Khuda Bakhsh, kwenye makaburi ya familia yaliyogeuka kuwa eneo takatifu la kisiasa.

Benazir Bhutto anabaki kwenye historia kama nembo ya mwanamke aliyevunja minyororo ya mfumo dume wa kisiasa. Licha ya mapungufu ya kiutawala na tuhuma zilizomkabili, ujasiri wake wa kuwaangalia wauaji wake machoni na kukataa kuacha kupigania kile ali-chokiamini, unamfanya abaki kama mshumaa wa demokrasia uliokataa kuzimwa na vitisho, akiyatoa maisha yake kama sadaka kwa ajili ya watu wake.

MUHIMU: Makala haya ya historia yamechapishwa kwa mara ya kwanza na #theconnect. Pambazuko limechota na kuchapisha kutokana na umuhimu wake kuonyesha uwezo wa wanawake.

■ Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

Vyombo vya habari vinahitaji PR

KUNA dhana ya ajabu imejengeka mitaani, watu wanadhani mtu akiwa na kipaza sauti au kamera, basi tayari kashaimaliza kazi ya kuji-tangaza.

Wanadhani chombo cha habari hakihitaji chochote zaidi ya kuripoti habari za watu wengine.

Nataka niwaambie jambo moja leo kwamba kwa uzoefu wangu katika fani hii ya Uhusiano na Umma na Mawasiliano (PR), hilo ni wazo la mtu ambaye hajawahi kukaa chumba cha mikutano cha bodi ya wakurugenzi wa gazeti au kituo cha runinga wakati mauzo yameshuka na wafadhili wanauliza maswali magumu.

Redio, runinga na magazeti ni biashara, ni chapa na ni bidhaa inayouzwa sokoni kama sabuni au soda.

Tofauti pekee ni kwamba bidhaa yao ni imani ya watu, ukiuza imani lazima uwe na mtu wa kuilinda imani hiyo. Hapo ndipo PR inapoingia, na wala siyo kwa maandamano au sherehe za uzinduzi tu.

Vyombo vya habari vinaripoti mambo ya kisiasa yenye hisia kali, vinachapisha habari za uchunguzi zinazogusa watu wenye nguvu, wakati mwingine vinakosea kabisa kwenye tarifa na kulazimika kurekebisha.

Ukikosea kama gazeti au kituo, wewe mwenyewe umekuwa habari, sasa wewe uliyekuwa unaandika habari za wengine, leo ni wewe ndiye unayeandikwa ama kutangazwa.

Ukiwa huna mtu aliyejipanga vyema kukusimamia katika kipindi hicho, watu watakumaliza kwenye mitandao kabla hujajua kinachoendelea.

Hapa ndipo PR ya chombo cha habari inapofanya kazi yake halisi, siyo kufunika makosa.

Ni kuhakikisha unaeleza upande wako wa habari bila “kuongeza mafuta kwenye moto uliokwishawaka.”

Watu wengi wanadhani wateja wa gazeti ni wale wanaosoma habari, la hashu! Mteja mkubwa zaidi wa gazeti au kituo ni mfanyabiashara mwenye pesa za matangazo.

Chombo kisichojijenga kwa mikakati ya PR mbele ya wafanyabiashara kitabaki kikigombania matangazo madogo madogo huku wenzake wakichukua mikataba mikubwa ya muda mrefu.

Msomaji au mtazamaji anapenda chombo kwa sababu anakiamini, anaamini kinamwambia ukweli, anaamini hakiuzwi kwa yeyote mwenye bahasha nzito.

Imani hii haijengeki yenyewe, inajengwa kwa makusudi, kwa miaka mingi, kupitia kazi za kijamii, michango, tuzo za waandishi bora, na uhusiano wa karibu na jamii inayohudumiwa.

Mwandishi mzuri, mtangazaji mzuri, mhariri mzuri, hawapendi kufanya kazi mahali ambapo jina limeharibika. Hata ukimlipa vizuri kiasi gani, kama chombo kina sifa mbaya sokoni, mtaalamu makini atakwepa.

Enzi zile za redio kuongea na wewe kunyamaza zimepita, leo kuna mitandao, msikilizaji anaweza kujibu papohapo, anaweza kukosoa, anaweza kuunda ukweli wake mwenyewe kabla wewe hujamaliza sentensi yako.

PR ya sasa siyo tena taarifa kwa vyombo vya habari peke yake, ni jinsi unavyozungumza na kijana wa mtandaoni anayetazama TikTok bada-la ya runinga saa nne usiku.

Chombo kisichofahamu hili kitabaki kikijiuliza kwa nini vijana hawakioni tena, wakati jibu liko wazi kabisa mbele yake.

Basi ndugu zangu wa vyombo vya habari, msijidanganye, mkiwa mnadhani kazi yenu ni kutengeneza habari za wengine tu bila kujiangalia ninyi wenyewe kwenye kioo, siku moja mtaamka mmekuwa habari mbaya, na hakuna atakayewaokoa.

PR siyo anasa ya kampuni kubwa za simu na benki peke yake, ni silaha ambayo hata chombo kinachotengeneza habari kinahitaji kuwa nayo mfukoni, tayari kwa siku ambayo dunia itataka maelezo.

Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz

Na Emmanuel JACOB



Afya ya Kimwili ■

Maumivu yakizidi mwilini ubongo huibuka

JE, umewahi kupata maumivu makali ya mwili kama vile mgongo au kichwa kisha akili yako ikaanza kukuambia, “Haya maumivu hayatakaa yaishe, na hakika nitapooza”?

Kimsingi, maumivu ni ishara ya kibiolojia inayotonyia kuwa kuna kitu hakiko sawa mwilini. Hata hivyo, jinsi tunavyoyawazia maumivu hayo inaweza kuwa kichocheo kikubwa cha kuyaongeza au kuyapunguza.

Mtindo usiofaa wa kufikiri unaoitwa pain catastrophizing (Kiswahili tunaweza kuuita kukuza fikra za maumivu). Huku ni kule kuwazia maumivu katika picha hasi zaidi kuliko uhalisia ulivyo.

Mtindo huu wa kisaikolojia una sehemu kuu tatu.

Kwanza, kukuza mambo kuliko uhalisia. Hii ni kufanya maumivu yaonekane kama janga kubwa. Mgonjwa anaweza kujikuta anawaza: “Maumivu ninayopata ni makali mno, na hakuna mtu aliyewahi kuumwa hivi duniani.”

Badala ya kuona maumivu kama changamoto ya kawaida ya kiafya inayoweza kutibika, akili inayakuza na kufanya yaonekane kama mlima mrefu usioweza kupandika, anawaza jambo baya litamtoka.


Pili, msongamano wa mawazo bila suluhisho. Hali hii hutokea pale akili inaponaswa na maumivu kiasi cha kushindwa kufikiria kitu kingine chochote.

Mtu anashindwa kabisa kujinasua kutoka kwenye mawazo ya ugonjwa ili kuendelea na kazi, mazungumzo au kufurahia maisha na familia. Maumivu yanakuwa ndio malalamiko kila sekunde ya maisha yake.

Tatu, kukata tamaa kabisa. Hii ni hisia hatari ya kuona kwamba huna nguvu wala uwezo wowote wa kubadili hali yako.

Mgonjwa anajawa na fikra kwamba: “Hakuna kitu chochote kinachoweza kupunguza maumivu haya na hakuna daktari au dawa itakayosaidia.” Hali hii inamfanya mtu ajisikie mnyonge na kupoteza matumaini ya kupona.

Unapokuza fikra za maumivu, ubongo unazalisha vichocheo vya msongo wa mawazo ambavyo kwa



uhalisia huongeza ukali wa maumivu hayo mwilini.

Habari njema ni kwamba, mtindo huu wa kufikiri unaweza kubadilishwa. Kupitia muongozo wa mtaalamu utajifunza mbinu mbalimbali za kutuliza akili, vilevile kutotafsiri kila maumivu kama mwisho wa dunia.

Siku moja, bibi mmoja alikuja kliniki na kuniambia; “Mgongo wangu niliambiwa pingili zimesagika na mimi ni mzee”. Maneno hayo na mengine aliyo-tumia yalionyesha wazi anavyofikiri ile kusagika ni kana kwamba mgongo wake si imara tena na hatapata nafuu tena.

Mara nyingi ninapenda kutumia mbinu mbalimbali, ikiwemo mifano, ili kubomoa misingi ya hofu na kujenga hisia za kiusalama na kujiamini.

Nilicheka halafu nikasema: “Bibi, hivi mvi kichwani nazo zinamaanisha nywele zako zimeharibika?”

Alishtuka na kucheka kwani hakutegemea. Nili-chokuwa namaanisha ni kuonyesha kuwa mabadiliko ya miili yetu (ikiwemo diski na pingili), hayamaanishi kwamba miili yetu imeharibika kabisa na haiwezi chochote.

Ni muhimu kubadili mtazamo na kutokuhusisha kila dalili na uzee au mwisho wa uwezo wako wa kufanya mambo.

Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Ameandika Kitabu cha Mbinu za Kutibu Maumivu Sugu). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob.

■ Bustani ya Sheria



Na Karim Gabriel Mussa

Kesi iliyobadili sheria ya mgawanyo wa mali za ndoa



MWAKA 1983, Mahakama ya Rufani ya Tanzania ilitoa uamuzi uliobadili kabisa mtazamo kuhusu haki za wanawake katika mali za ndoa.

Katika shauri la Hawa Mohamed dhidi ya Ally Sefu (Civil Appeal No. 9 of 1983), mahakama ilifafanua kuwa kazi za nyumbani ni mchango halali unaostahili kutambuliwa wakati wa kugawa mali za ndoa.

Baada ya ndoa ya Hawa Mohamed na Ally Sefu kuvunjika mwaka 1980, mzozo ulizuka kuhusu mgawanyo wa nyumba waliyoishi.

Mahakama ya Mwanzo iliamua kuwa Hawa hakuwa na haki ya nyumba hiyo kwa sababu hakuchangia fedha katika kuinunua, na ikaamuru apewe Shilingi 3,000 tu. Rufaa yake Mahakama Kuu ilikataliwa, hivyo akaamua kukata rufaa Mahakama ya Rufani.

Hoja kuu ilikuwa tafsiri ya neno “contribution” chini ya Kifungu cha 114 cha Sheria ya Ndoa, Sura ya 29. Upande wa mume ulidai mchango unaotambulika ni wa fedha au kazi ya moja kwa moja katika kupata mali.

Hawa, kwa upande wake, alieleza kuwa kwa miaka yote alikuwa akilea watoto, akipika, akifanya usafi na kutunza familia, jambo lililomwezesha mume wake kufanya kazi na kujenga mali.

Mahakama ya Rufani, chini ya Jaji Mkuu Francis Nyalali na wenzake, ilikubaliana na hoja hiyo. Ilisisitiza kuwa ndoa ni ushirikiano, na kazi za nyumbani zina thamani sawa na mchango wa kifedha. Hivyo, mwanamke wa nyumbani hawezi kunyimwa haki ya mali za ndoa kwa sababu tu hakupata mshahara.

Hata hivyo, Hawa hakupata sehemu ya nyumba aliyokuwa anadai. Mahakama ilibaini kuwa kabla ya ndoa kuvunjika alikuwa amondoka nyumbani na kuishi na mwanaume mwingine, kitendo kilichoonekana kuwa ni ukiumkaji mkubwa wa wajibu wa ndoa.

Kutokana na mwenendo huo, mahakama iliona hakuwa na sifa ya kugawiwa nyumba hiyo.

Licha ya matokeo hayo, kesi hii imebaki kuwa msingi muhimu wa sheria za familia nchini. Ilithibitisha kuwa kazi za nyumbani ni mchango wa kweli katika upatikanaji wa mali za ndoa, huku ikikumbusha kuwa mwenendo wa wanandoa unaweza pia kuzingatiwa wakati wa kugawa mali baada ya ndoa kuvunjika.

Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbimussa@gmail.com

Na Rashid MTAGALUKA



Hoja Yangu ■

Tusiache kueleza machungu ya historia miaka 100 ya Bunge

KAULI ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mussa Zungu, mbele ya wahariri kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya miaka 100 ya chombo hicho, imefungua ukurasa muhimu wa kutafakari historia ya taasisi hii.

Lakini, katika taifa linalojenga misingi ya uwajibikaji, maadhimisho ya karne moja hayapaswi kuwa ya kushangilia pekee. Yanapaswa kuwa ya kuuliza maswali magumu.

Baada ya miaka 100, je, Bunge limebaki kuwa sauti ya wananchi au limeonekana zaidi kama muhuri wa uamuzi wa serikali? Hili ndilo swali ambalo Watanzania wengi wangependa kulisikia likijibiwa kwa vitendo badala ya kauli za kisiasa.

Hakuna ubishi kuwa Bunge limepitisha sheria nyingi, limejadili bajeti za mabilioni ya shilingi kila mwaka, limeunda kamati za kudumu na kuwahoji mawaziri kuhusu matumizi ya fedha za umma.

Hata hivyo, kipimo cha mafanikio ya Bunge siyo idadi ya sheria zilizopitishwa, bali ni athari zake katika maisha ya mwananchi wa kawaida.

Kwa miaka mingi, baadhi ya ripoti za Kamati za Bunge zimebaini ubadhirifu wa fedha za umma, ucheleweshaji wa miradi na ukiukwaji wa taratibu katika taasisi mbalimbali, lakini mara nyingi wananchi wamejiuliza, ni mapendekezo mangapi yametekelezwa kikamilifu?

Je, ni viongozi wangapi waliowajibishwa kutokana na hoja zilizobainishwa na Bunge? Bila majibu ya maswali hayo, kazi ya Bunge inaweza kuonekana kuwa ya kutoa maonyo kuliko kuleta mabadiliko.

Aidha, dhana ya mgawanyo wa madaraka ndiyo msingi wa utawala wa kidemokrasia. Bunge linapaswa kuisimamia serikali bila kuyumba.

Pia, kumekuwa na mijadala ya muda mrefu kuhusu iwapo nguvu ya chama chenye wabunge wengi imeathiri uhuru wa mijadala na uwezo wa wabunge kuikosoa serikali kwa kiwango kinachotarajiwa. Huu siyo mjadala wa kupuuzwa,

bali ni sehemu ya afya ya demokrasia.

Je, mikataba mikubwa inapata uchambuzi wa kutosha? Je, sheria zinazopitishwa zinatanguliza maslahi ya vizazi vijavyo? Haya ni maswali yanayohitaji majibu ya wazi.

Miaka 100 pia ni nafasi ya kutathmini uhusiano kati ya Bunge na wananchi, licha ya maendeleo ya teknolojia, bado wananchi wengi hawafuatilii mijadala ya Bunge wala hawaelewi kwa kina sheria zinazopitishwa. Hilo linapaswa kuwa changamoto kwa Bunge kuongeza uwazi, kurahisisha upatikanaji wa taarifa na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika mchakato wa kutunga sheria.

Kwa vyombo vya habari, maadhimisho haya ni mwito wa kufanya zaidi ya kuripoti sherehe. Ni wakati wa kuchunguza historia ya sheria zilizoleta mabadiliko makubwa, kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge na kuhoji kama taasisi hiyo imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kikatiba bila kuyumbishwa na mazingira ya kisiasa.

Hakika, Bunge la Tanzania linastahili heshima kwa kufikisha miaka 100. Lakini heshima ya kweli ya taasisi yoyote ya kidemokrasia haipimwi kwa umri wake, bali kwa kiwango cha imani ambacho wananchi wanayo kwake.

Imani hiyo hujengwa na uwajibikaji, uwazi, ujasiri wa kusimamia maslahi ya umma na utayari wa kuikosoa serikali pale inapokosea.

Ndiyo maana maadhimisho ya miaka 100 yanapaswa kuwa mwanzo wa safari mpya ya kujitathmini, badala ya kuwa mwisho wa simulizi la kujisifu.

Historia ni muhimu, lakini historia itakuwa na thamani zaidi ikiwa itatumika kujenga Bunge lenye nguvu zaidi, huru zaidi na linaloaminika zaidi katika karne ijayo.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com

■ Habari katika Picha



Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu akiwa Mahakama ya Rufani alipoletwa kutoka gerezani kusikiliza maombi ya marejeo ya kuongeza ushahidi yaliyowasilishwa na DPP katika kesi yake ya uhaini inayomkabili, jijini Dar es Salaam juzi. (Picha na Kamera ya Pambazuko).



Dereva wa daladala linalofanya safari zake kati ya Makumbusho na Gerezani, akiwa amevaa sare zake vibaya kinyume na sheria za usafirishaji zinavyoelekeza kama alivyokutwa na kamera ya Pambazuko, jijini Dar es Salaam jana.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Augustino Senga akimkabidhi zawadi mmoja wa wazazi waliojifungua katika Hospitali ya Vwawa Wilaya ya Mbozi mkoani humo alipotembelea na kutoa zawadi kuadhimisha kumbukizi ya miaka 10 ya utumishi, mwishoni mwa wiki. Picha na Issa Mwadangala.

Mabasi yakiwa yameegeshwa kwenye hifadhi za Barabara ya Morogoro ambazo sasa madereva wamezigeuza kuwa stendi za kushusha na kupakia abiria na kusababisha kero kwa watumiaji wengine eneo la Shekilango jijini Dar es Salaam jana. (Picha na Kamera ya Pambazuko).



Bati/ Mtu, Mtu Bati HATUCHOKI!



Changia kupitia

NMB A/C NO 31910046325

ELCT KARAGWE IRON SHEET PROJECT


CRDB A/C NO 0150764151900

UWAKILI PROJECT ELCT KAD

Mawasiliano:

0754 742 423

Askofu Benson K Bagonza



Siku maalumu huimarisha ndoa

HABARI msomaji wa safu ya uhusiano. Karibu uweze kujipatia elimu kuhusu uhusiano katika nyanja mbalimbali.

Wiki hii nitazungumza namna matukio muhimu kwa wanandoa yanavyoweza kustawisha ndoa yao.

Ndoa inahitaji zaidi ya kuishi pamoja kila siku. Inahitaji vituo vya kukumbusha kwa nini mlipendana na kuamua kuwa mwili mmoja.

Matukio kama siku ya kuzaliwa, kumbukumbu ya ndoa, mafanikio ya kazi, na hata siku ya kawaida ndio hufanya kazi hiyo.

Maisha ya ndoa yanaweza kuonekana yanachosha hasa kunapokuwepo mazingira yaleyale miaka nenda rudi.

Mwaka ukipita bila kituo chochote maalum, upendo unazoeleka na kuanza kuonekana kama wajibu wenye kuchosha.

Kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa inaweza kusimamisha huo mzunguko kwa saa 24.

Siku hiyo maalum inasema kwa vitendo kuwa leo hatutazungumza bill au kazi, bali ni wewe tu. Hilo linarejesha msisimko wa siku za mwanzo mlipoanza uhusiano.

Matukio haya pia yanajenga benki ya kumbukumbu ambayo ndoa inakula wakati wa ugumu.

Ubongo wetu unakumbuka hisia zaidi ya vitu ghali.

Keki moja uliyoshiriki, barua fupi ya mikono miwili, au kutembea pwani usiku ukila viazi vya Shilingi 2,000 vinaweza kuwa na uzito mkubwa kuliko zawadi ya aghali.

Miaka mingi baadaye mtaketi mkicheka na kusema, unakumbuka siku ile? Hizo ndizo akiba za moyo hivyo wanandoa mnapaswa kuenziana kwa vitu vya aina hiyo.

Kukumbuka siku ya mwenzi ni uthibitisho wa kimya kuwa bado unamchagua. Kumshangilia bila kukumbushwa kunafuta hofu hiyo.

Uwepo wa matukio haya huponya majeraha madogo ya wiki nzima ya migogoro kwa neno moja la shukrani.

Siri siyo pesa nyingi, ni nia safi, muda, na umakini. Kumbuka, sikiliza ambacho mwenza wako anakipenda na mpe muda usiovurugwa. Ndoa inastawi kwa matukio madogo ya dhiti yanayorudiwa, sio makubwa ya mara moja.

Ukitaka kuifanya ndoa yako kustawi na kushamiri tumia mbinu hizi, hakika utafurahia daima, Anza sasa.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.

Mitindo & Urembo ■

Teyana kwenye gauni la kifahari BET Awards 2026

MWANAMITINDO na mwana-muziki, Teyana Taylor ameibuka kuwa mmoja wa walioteka “Zuria Jekundu” kwenye BET Awards 2026.

Teyana aliwasili akiwa amevaa vazi bora ya kipekee iliyoungwa kwa ubunifu wa hali ya juu na kwa ustadi mkubwa wa mikono.

Vazi hilo lilibuniwa na Stephane Rolland SS26 Couture.

Gauni lake la rangi ya “burgundy” ambalo halina kamba za mabega wala miko-no iliyobana vizuri mwilini na kuonekana kuwa la ubunifu wa kisanaa, liliwavutia macho ya wengi.

Muonekano huo ulikamilishwa na pambo la kichwa lililoundwa kwa muundo wa duara inayolingana na rangi ya gauni pamoja na mtindo wa nywele ulionyooka vizuri.

Mbali na kung’ara kwa staili yake, Teyana Taylor pia alitunukiwa heshima ya BET Icon of the Year 2026, na kufanya usiku huo kuwa miongoni mwa nyakati muhimu zaidi kwenye safari yake ya muziki, mitindo na burudani.



Tumia parachichi kutunza ngozi yako

PARACHICHI ni tunda lenye utajiri wa Vitamini A, C na E, hivyo ni nzuri sana kwa ngozi yako kwa sababu ina mafuta asilia yanayosaidia kulainisha ngozi.

Pia tunda hilo linasaidia kuondoa mikunyo na kuzuia uharibifu unaotokana na miale ya jua.

Matumizi

Pondaponda parachichi kisha uchanganye na asali kijiko kimoja halafu upake mchanganyiko huo usoni, acha kwa dakika 10 kisha safisha uso wako.

Kwa matokeo mazuri zaidi, tumia mara mbili kwa wiki.

■ Burudani



Matonya aachiwa huru kesi ya ubakaji

Na Mwandishi WETU

MAHAKAMA ya Shanzu, Kaunti ya Mombasa nchini Kenya, imemuachia huru msanii wa muziki kutoka Tanzania, Seif Ramadhan maarufu Matonya aliyekuwa anakabiliwa na kesi ya ubakaji.

Akizungumza baada ya hukumu hiyo iliyotolewa Julai 2, 2026, Matonya alitoa shukrani kwa mashabiki, familia yake na wote walio muunga mkono katika kipindi chote cha kesi hiyo.

Mbali na kuachiwa huru, mahakama hiyo pia imeagiza arejeshewe passport yake iliyokuwa imezuiliwa wakati wa uendeshaji wa kesi.

“Ndugu zangu Wakenya, sikuwa tayari kupoteza upendo tuliojenga kwa zaidi ya miaka 19 na sijui limetokeaje, lakini nime wasamehe,” amesema Matonya.

Matonya alifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza Aprili 9, 2026, akikabiliwa na shtaka la ubakaji linalodaiwa kutokea Aprili 7, 2026 katika eneo la Josy, Nyali, Mombasa.

Alidaiwa kumbaka mwanamke aliyetambulishwa kwa herufi J.G.

Daveigh afariki na virusi vya Ukimwi

Na Mwandishi WETU

TAARIFA rasmi ya kifo cha mwigizaji wa filamu kutoka nchini Marekani, Daveigh Chase, inaeleza kuwa kimetokana na magonjwa yanayochochea na virusi vya ugonjwa wa Ukimwi.

Daveigh alifariki Juni 18, 2026 akiwa anapatiwa matibabu huko New York.

Taarifa zinaeleza kuwa pamoja na kwamba alikuwa na Ukimwi, lakini pia alikuwa akitumia dawa za kulevya, hatua

ambayo pia ilichangia kupoteza maisha.

Daveigh alianza kuigiza akiwa na umri wa miaka minne, alishiriki katika filamu mbalimbali ikiwemo ya The Ring.

Pia sauti ya Daveigh ilitumika kwenye katuni ya Lilo and Stich, yeye akiwa kama Lilo.

Daveigh amefariki akiwa na umri wa miaka 35, wazazi wake walisema siku za mwisho za maisha yake, mwigizaji huyo hakuwa na makazi maalumu alikuwa akiishi mtaani na mpenzi wake.

Na John Marwa



Kombe la Dunia

Kiungo mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Morocco, Azzedine Ounahi akibebwa na wachezaji pamoja na viongozi wa timu hiyo baada ya mechi ya hatua ya 16 bora dhidi ya Canada kumalizika kwa ushindi wa 3-0 juzi. Mchezaji huyo alifunga mabao mawili. (Picha na AP)



Notisi za Cape Verde wapewe Morocco, Misri

TIMU ya Taifa ya Cape Verde imeacha kumbukumbu ya kishujaa kwa wapenzi wa kandanda kote duniani kwa kuonyesha kiwango bora kwenye Fainali za 23 za Kombe la Dunia 2026, zinazoendelea Marekani, Canada na Mexico.

Siyo kinyonge kwa vijana wa kisiwa cha miujiza - Cape Verde licha ya kuondoshwa katika hatua ya 32 na Argentina, wao wameishinda mioyo ya mamilioni wa masahabiki wa soka kwa kuonyesha hadhi ya nyota tano ikiwa ni mara ya kwanza taifa hilo kushiriki mashindano hayo makubwa ya soka.

Cape Verde – almaarufu 'Blue Sharks' ni taifa dogo watu wenye mioyo mikubwa ya kupambana na wapiganaji wa kweli, miongoni mwa rekodi walizoondoka nazo ni kutopoteza mchezo katika hatua ya makundi huku katika michezo minne hawakupoteza mchezo ndani ya dakika 90.

Michezo mitatu ya kundi H, walitoka suluhu

dhidi ya Hispania na dhidi ya Saudi Arabia, pia wakatoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya mabingwa wa kihistoria Uruguay. Mbele ya Argentina ndani ya dakika 90 (1-1), dakika 105 (2-2) na dakika 120 (3-2).

Hadi sasa Afrika bado ina tabasamu ingawa linachoma mioyo hasa kwa Waafrika weusi ambao wawakilishi wa mataifa yao yote yameondoshwa huku wakisalia wenzao kutoka kaskazini; Morocco na Misri hatua ya 16 bora.

Morocco wao wametinga hatua ya robo fainali na mbele yao ni timu ya Taifa ya Ufaransa, mchezo unaoweza kutajwa kuwa umebeba kisasi kwani katika mzunguko wa 22, miamba hiyo ilikutana hatua ya nusu fainali na Wafaransa wakawaondosha Morocco kwa mabao 2-0 nchini Qatar 2022.

Misri nao wana kazi ya kufanya kesho - Julai 7 dhidi ya mabingwa watetezi Argentina ya Lionel Messi, kusaka tiketi ya robo fainali.

Mtanange ambao unaweza kutazamwa kwa jicho pevu kutokana na mateso waliyapitia Argentina dhidi ya Cape Verde kwenye mchezo wa 32 bora licha ya kufanikiwa kushinda kwa mabao 3-2.

Sasa basi, ni vyema mbinu za uwanjani walizonazo Cape Verde wakawapa Waafrika wenzao ambao wanatinga robo fainali sasa ili Afrika iendelee kung'ara.



Steve Barker ni 'Mnyama'



Na John Marwa

KAMA una swali basi uliza, kama una hoja ilete mezani, kama unapenda futiboli keti na mtaalamu Steve Barker akufundishe namna utulivu, nidhamu vinapozaa ushindi katika kila dakika 90 za kandanda.

Ni Steve Barker, Kocha wa Mabingwa wa Kombe la Shirikisho 'CRDB Federation Cup'

Simba. Huyu anaweza kutajwa kuwa ni mkombozi wa makombe.

Hivyo ndivyo unaweza kueleza mara baada ya msimu wa mashindano 2025/26 kumalizika huku Simba akinyanyua kwapa mara mbili na furaha ya mataji kurejea Msimbazi.

Kocha huyo mzaliwa wa Maseru, Lesotho mwenye uraia wa Afrika Kusini, ni mpwa wa kocha mashuhuri, Clive Barker aliyeiongoza Bafana Bafana kutwa Afcon 1996.

Steve Barker ameiongoza Simba kwa miezi sita na kufanikiwa kuwasha taa ya kijani katika ramani ya kurejesha makombe Msimbazi.

Aprili mwaka huu - 2026, Kocha Barker aliiongoza Simba kutwaa ubingwa wa Kombe la Muungano, fainali iliyopigwa Unguja, visiwani Zanzibar kwa kuwafunga watani wao wa jadi, Yanga kwa bao 1-0 kwa njia ya mkwaju wa penati uliowekwa kimiani na Seleman Mwalimu 'Gomez'.

Tena, Julai 4, 2026 akarejesha taji la Shirikisho la CRDB kwa kuwafunga Azam, fainali iliyopigwa Pemba visiwani Zanzibar, kwa bao 1-0, na kuhitimisha msimu na mataji mawili kabatini kutoka Unguja na Pemba.

Sasa swali linatanda; kwamba je, safari na kituo kijacho cha kuchukua mataji ni Tanzania Bara kwa msimu ujao kwenye michuano ya ligi kuu?

Swali hilo linasubiri majibu ndani ya mkataba wake wa miezi 18 iliyosalia ikiwa mabosi wa Simba hawatamungezea mkataba zaidi, basi msimu 2026/27 ana kazi ya kurejesha kombe hilo walilolipoteza mara tano mtawalia kwa watani zao Yanga.